**Metropolitan Journal of Social and Educational Research (MJSER)**

**ISSN 1813-4262 (Print)**

**ISSN 1813-4270 (online)**

**Vol. 2 Issue 2, May - 2023, Pages: 936-945**

# *MCHANGO WA KUTUMIA VYOMBO VYA HABARI KATIKA KUENEZA LUGHA YA KISWAHILI NCHINI UGANDA: ENEO LA MUNISPALI YA NANSANA*

***1 Magezi Adinari, 2 Mukoyani Geophrey***

***1, 2 Shule ya Metropolitan International University***

***MUHTASARI***

*Utafiti uliolenga mchango wa kutumia vyombo vya habari katika kueneza lugha ya kiswahili nchini Uganda na iliongozwa na maswali yafuatayo Kutathimini sababu zinazofanya Kiswahili kisitumike katika kutangaza habari na vipindi, Kutambua maoni kwa nini wananchi hawaelewi lugha ya Kiswahili na Kuchunguza athari za vyombo vya habari katika lugha ya Kiswahili nchini Uganda. Kiswahili kinatambulika kama lugha ya Afrika Mashariki. Kwa miaka mingi sasa imekuwa ikipata hadhi ya lugha ya Kimataifa, licha ya kwmba imekuwa ndio njia kuu ya mawasiliano baina ya watu wa makabila tofauti. Sifa hizi zote ni ushahidi wa haraka tu kwamba Kiswahili ni lugha ambayo imeweza kujenga misingi maalum ya maarifa ya wazungumzaji wake. Hii inatokana na kuwa hizi ni sifa zinazodhihirisha kuwa Kiswahili kinaweza kuzielezea dhana tofauti za watu wa aina mbalimbali na zikaeleweka kwa wazungumzaji wengine na hivyo watu kuelewana. Mtafiti alitembelea ofisi mbalimbali za vyombo vya habari na kuhojiana nao ambapo jumla ya watalaamu sitini aliowatembelea walisema Lugha ya Kiswahili inafaa kutumika kutolewa habari vyomboni vya habari, ambapo matokeo yalikuwa kama ifuatavyo, asilimia 80 walisema inafaa, asilimia 05 walisema haifai kutumia kiswahili kama lugha ya kutolewa habari na asilimia 15 walisema lugha zote ni sawa. Tamko la serikali kuhusu matumizi ya lugha ya kiswahili katika shughuli za umma. Kiswahili ndio lugha pekee ambayo huzungumzwa na kueleweka na idadi kubwa zaidi ya watanzania nchini kote.*

**Metropolitan Journal of Social and Educational Research (MJSER)**
**ISSN 1813-4262 (Print)**
**ISSN 1813-4270 (online)**
**Vol. 2 Issue 2, May - 2023, Pages: 936-945**

*Maneno muhimu:* ***kutumia vyombo na mchango***

## *UTANGULIZI*

*Mchango ni umuhimu wa kitu Fulani na kwahivyo mchango wa vyombo vya habari katika kueneza lugha ya Kiswahili. Unaangaliwa kupitia chombo chenyewe Fulani kwa kutoa vile tunavyo saidia kukunza lugha. Vyombo vya habari ni vyombo vya mawasiliano vinavyolenga watu wengi kuwapatia habari au burundani. Mashirika ya habari mara nyingi ni lengo lao hutarajiwa kuwa usawa, waandishi hudai kwamba wao hujaribu kufua pande zote za suala bila mapendeleo na watangazaji au wachambuzi ambao hutoa maoni au dhana ya kibinafsi. serikali nyingi zenye chama moja zinaendesha mashirika ya habari, ambayo yanaweza kuwasilisha maoni ya serikali. vyombo vya habari ni sehemu ya habari tu ambayo huonyesha jumla ya maendeleo duniani. Kuna wataalamu wanaojumlisha pia vitabu katika historia ya vyombo vya habari tangu kupatikana kwa uchapishaji vitabu, wengine wanaona pia aina za maigizo ya tamthilia kama vyombo vya habari katika jamii za kale. Katika nchi uganda kuna aina mbalimbali ya vyombo vya habari kama magazeti, redio, televisheni, mtandao, magazini. Huduma hizo hujumuisha kuwafundisha, kuwajuza, kuwaburundisha na hata kuelimisha jamii kwa namna moja au nyingine kuhusu mbinu za lugha ya Kiswahili. Makala haya yanatathmini juhundi za vyombo vya habari katika kukuza na kueneza Kiswahili nchini uganda kwa kujikita katika gazeti la taifa leo, idhaa za redio (UBC REDIO) pamoja na kituo cha runinga UBC. (Mnyampala 2015)*
*Haki hii, kama zilivyo haki nyingine zote, hutolewa kwa kuzingatia wajibu wa kila raia kwa jamii na uhuru binafsi wa binadamu. Dhima ya Sekta ya Habari na Utangazaji katika jamii ni kutoa habari, kuelimisha na kuburudisha. Sekta hii inahudumiwa na vyombo vya habari ambavyo ni redio, magazeti, majarida, televisheni, filamu, video, intaneti, picha, vipeperushi, katuni na mabango.*

## *Tatizo la Utafiti*

*Tatizo lililomfanya mtafiti afanye utafiti huu ni, "kuchanganua mchango wa utumiaji wa vyombo vya habari katika kueneza lugha ya kiswahili nchini uganda". Katika kuliendeleza*

*Taifa, Mtafiti aliamua kufanya utafiti huu baada ya kugundua kwamba vyombo vya habari kadhaa vimesaidia katika kuienzi lugha ya Kiswahili nchini Uganda ingawa Kiswahili bado hakijafanywa lugha rasmi. Halliday (2018) lugha inaweza kutafitiwa katika muktadha yake.*

*Tatizo lingine lililomfanya mtafiti afanye utafiti huu ni kwa kuzingatia kuwa lugha ndiyo utambulishi wa utamaduni. Lugha na utamaduni ni vitu viwili vinavyohusiana na visivyotenganishika. Pamoja na ukweli huu, bado Uganda haijafanya uamuzi wa kutumia Kiswahili katika program na Kusoma habari katika vyombo vya habari nchini. Kwa muktadha huu utafiti ulijikita katika kuainisha sababu zinazokwamisha kufikiwa kwa uamuzi juu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kutangaza vipindi kadha kwenye vyombo vya habari hapa uganda, pamoja na kuwepo utoshelevu usiotiliwa shaka yoyote.*

### *Malengo Mahususi*

1. *Kutathimini sababu zinazofanya Kiswahili kisitumike katika kutangaza habari na vipindi.*
2. *Kutambua maoni kwa nini wananchi hawaelewi lugha ya Kiswahili.*
3. *Kuchunguza athari za vyombo vya habari katika lugha ya Kiswahili nchini uganda.*

### *Maswali ya Utafiti*

*Kufikia lengo kuu na malengo mahususi ya utafiti huu, mtafiti alitoa maswahili mbalimbali kwa watafitiwa ili yajibiwe. Yafuatayo ni maswali yaliyoulizwa na mtafiti.*

1. *Ni kwa nini Kiswahili hakitumiki katika utangazaji wa habari na vipindi?*
2. *Ni kwa nini wananchi hawaelewi lugha ya kiswahili?*
3. *Ni vyombo vya habari katika kueneza lugha ya kiswahili nchini Uganda?*

## *MBINU ZA UTAFITI*

### *Mbinu ya Umakinifu au Shirikishi*

*Kuhusu utekelezaji wa kuzikusanya data kwa njia Shirikishi, Mtafiti aliwateua wanahabari, na wakazi wa eneo la utafiti huu yaani wilaya ya kampala. Utafiti kuhusu "**mchango wa utumiaji wa vyombo vya habari kueneza lugha ya kiswahili nchini uganda"** Jumla*

**Metropolitan Journal of Social and Educational Research (MJSER)**
**ISSN 1813-4262 (Print)**
**ISSN 1813-4270 (online)**
**Vol. 2 Issue 2, May - 2023, Pages: 936-945**

*kulikuwa na watafitiwa sitini (60) kwa watafitiwa wote.*

***Mbinu ya Maktaba***

*Mtafiti alisoma kazi tangulizi katika maktaba mbalimbali nchini hususani maktaba ya, chuo kikuu cha kimataifa cha metropolitan, chuo kikuu cha kimataifa cha kampala, chuo kikuu cha makerere, chuo kikuu cha kampala, chuo kikuu cha Kyambogo na maktaba nyinginezo nyingi. Katika maktaba, mtafiti anasoma magazet, majarida, na vitabu. Maktaba hizi mtafiti alipata matokeo ya wananchi. Mtafiti alizichagua maktaba hizi kwa kuwa zipo karibu na mazingira ya mtafiti kwani mtafiti anaishi mtaa Namungoona.*

*Zina taarifa nyingi zinazohusu utafiti wa mtafiti.*
*Ni rahisi kufikika kupata taarifa mbalimbali za mtafiti.*
*Wahusika au watafitiwa wanapatikana maeneo hayo.*

***Usaili***

*Mtafiti aliandaa maswali ya ana kwa ana na kuandika ambayo aliyatumia katika kupata majibu ya maswali ya utafiti. Maswali hayo yameambatanishwa kwenye kiambatanisho nyuma.*

***Hojaji***

*Mtafiti aliwateua wanahabari na wakazi katika eneo la utafiti huu ambapo jumla ya watafitiwa watakuwa [40] ambapo wanahabari watakuwa kumi (10) na wakazi watakuwa thelathini (30)*

***Ukusanyaji wa Data***

*Ukusanyaji wa Data ni namna ya kutafuta taarifa mbalimbali zenye ukweli ndani yake (Kombo na Tromp 2016). Katika utafiti huu njia zilizotumika zilikuwa ni Umakinifu au ushirikishi, Maktaba, Usaili/udadisi, Hojaji au mahojaji, Baraza la Mitihani. Mtafiti alikwenda ofisi za wilaya ya kampala na kupatiwa taarifa za idadi ya watu wa wilaya ya kampala pamoja na Shughuli za kiuchumi zinazofanywa katika wilaya ya kampala. Mtafifiti aliongea na wazee wa wilaya ya kampala na waliweza kuambiwa historia ya wilaya ya kampala.*

**Metropolitan Journal of Social and Educational Research (MJSER)**
**ISSN 1813-4262 (Print)**
**ISSN 1813-4270 (online)**
**Vol. 2 Issue 2, May - 2023, Pages: 936-945**

***Vikwazo vya Utafiti***

*Ilikuwa tarehe 26.9.2022, mtafiti alikwenda ofisi ya wilaya ya wakiso kukusanya taarifa, lakini alifika aliambiwa aone Afisa taaluma ili apate taarifa za kielimu za wilaya hiyo, Baada ya kumuendea taaluma alimwambia hawezi kumpatia taarifa za taaluma hapo ofisini kwani ni nyaraka za siri suala ambalo linaniumiza sana. Mtafiti ilimlazimu apite kila shule kuchukua taarifa hizo za masomo kwa walimu.*
*Itakuwa tarehe 21.9.2022, mtafiti atakuwa akielekea Mvomero kwa ajili ya Utafiti wake kukusanya data ataibiwa kamera kwenye gari na kusababisha ashindwe kupiga picha za matukio kwenye utafiti wake.*

***Mapendekezo***

*Mtafiti alipendekeza lugha ya Kiswahili itumike katika vyombo vya habari kutokana na kuwa ni lugha inayofaa kwa wananchi kutumiwa kama chombo cha mawasiliano.*

***Hitimisho***

*Katika sura hii ya tatu tuliwasilisha mbinu mbalimbali za ukusanyaji wa data ambapo data za awali na upili zilikusanywa. Data za awali zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usaili, hojaji na ushikishaji wa watafitiwa. Mbinu ya upitiaji wa machapisho ndio ilitumika katika kukusanya data za upili. Sura ifuatayo ilifanya uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti.*

***UCHAMBUZI WA DATA***

***Utangulizi***

*Mwandishi maarufa wa fasihi barani Africa, chinua achembe amewahi kutoa maoni haya kuhusu matumizi ya luhgha kama sanaa. [ imetabulikana tangu zamani kwamba lugha, kama ubunifu mwingine wowote wa wanadamu, inaweza kutumia vibaya, inaweza kugeuzwa kutoka mahimiziyake ya asilia na kufwa kitu kisicho na maana u hata chenye madhara. kauli hii ya Achembe inamaanisha kwamba lugha inaweza kutumiwa kwa njia potovu. Hata hivyo,*

**Metropolitan Journal of Social and Educational Research (MJSER)**
**ISSN 1813-4262 (Print)**
**ISSN 1813-4270 (online)**
**Vol. 2 Issue 2, May - 2023, Pages: 936-945**

*katiak uganda, kiwango cha ubora wa uandishi kwa jumla kimeshuka sana katika miaka ishirini iliyopita. makala hii ilichunguza kwa muhtasari ushaidi wa matumizi yasiyofaa ya lugha ya Kiswahili katika vyombo vya habari kwamfano redio, televisheni na magazeti.*

***Uwasilishaji wa data***

*Uwasilishaji na uchambuzi wa data uliefanyika kwa kuzingatia lengo kuu na malengo mahususi ya utafiti mada hii, na maswali yanayoambatana na malengo ya utafiti*

***Haja ya kutumia Kiswahili katika vyombo vya habari***

*Mwaka 2017 (Mlama & Matteru) Baraza la Kiswahili la Taifa lilidhamini utafiti uliofanywa na wataalamu wawili Mlama na Matteru. Wataalamu hawa walichunguza hali ya matumizi ya lugha ya kiswahili katika vyombo vya habari kutolea habari. Walitembelea vyombo vya habari katika mikoa kadhaa na kuzungumza na wanahabari na viongozi wa habari mikoani na wilayani. Walitoa pia hoja ambazo zilijazwa na wanahabari. Vile vile, walihudhuria vipindi radioni kwamfano 100.0 redio na nyingine. Katika utafiti huu, ilidhihirika bayana kwamba, stadi za lugha ya Kiingereza zimepungua kiasi kwamba mtindo wa kutuma lugha hiyo unatatiza wananchi. Matokeo ya hali hiyo ni kwamba hakuna ufanisi katika kufundisha na kujifunza.*

***Maoni ya Wananchi na Mwelekeo wa Mjadala***

*Maoni ya wataalamu wa elimu ni kuwa kiswahili ndio njia yenye ufanisi ya kutolea habari katika vyombo vya habari. Ukweli huu umethibitishwa na tafiti nyingi zilizofanywa pamoja na mahojiano yaliyofanywa hivi karibuni kati ya wanataaluma, BAKITA na wakufunzi wa vyuo mbalimbali.*

*Wanahabari na wananchi wanakiri kuwa kiswahili kipo katika hali mbaya na kwamba tatizo la kutoimudu lugha ya Kiswahili si la wanahabari tu, bali hata wananchi. Ingawa sera ya habari inawataka wanahabari kutolea habari yote kwa kiingereza isipokuwa somo la*

*Kiswahili, upo ukweli usiofichika kwamba wanahabari wengi wanatumia mchanganyiko wa Kiingereza na Kiswahili au wanaipuuzia sera hiyo na kutumia Kiswahili. Wanahabari wengi wanakiri kwamba, lugha ya Kiingereza imekuwa mzigo mzito na kikwazo kikubwa katika jitihada za kutoa habari.*

***Sababu Zinazofanya Kiswahili Kisitumike katika vyombo vya habari***

*Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, zipo sababu mbalimbali zinazofanya Kiswahili kisitumike kama lugha ya kutolea habari na matangazo katika ngazi ya vyombo vya habari nchini Uganda. Miongoni mwa sababu hizo ni ile inayodai kwamba Kiswahili ni lugha ya umoja hivyo ni wajibu kwa kila mwananchi ashughulikishe katika kusikiriza na kuzungumza lugha ya kiswahili kwa kupitia vyombo vya habari*.

***Mapendekezo kwa Serikali kuhusu matumizi ya kiswahili katika vyombo vya habari***

*Serikali ndio mdau mkuu wa sekta ya elimu chini na hivyo ina mamlaka ya juu katika maamuzi mbalimbali yanayohusu masuala ya elimu. Tunapendekeza kwamba serikali ifanye kila linalowezekana ili kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia elimu ya sekondari na kisha elimu ya juu.*

***Mapendekezo kwa Taasisi ya habari***

*Taasisi ya Elimu Tanzania ndio iliyopewa dhamana ya kukuza mitaala nchini. Hivyo kama sehemu ya wadau nchini inatakiwa ifanye utafiti wa kina juu ya lugha ya kufundishia ikishirikiana na wadau wengine ili kuweza kuishauri serikali ipasavyo juu ya lugha muafaka ya kufundishia. Iwapo taasisi hii itatoa ushauri sahihi kwa serikali basi itakuwa rahisi kwa serikali kutekeleza ushauri huo.*

***Mapendekezo kwa Vyuo vya habari***

*Nilipendekeza kwamba vyuo vikuu na vile vya ualimu ambavyo ndivyo vitoavyo walimu kuimarisha mitaala yao ili kuweza kupata walimu wabobezi katika lugha ya Kiswahili. Hii*

*itafanya kuwa si tu na walimu wa kutosha bali wenye uzoefu wa hali ya juu katika lugha ya Kiswahili.vile vile vitabu vyote vya vyuo vikuu vitafsiriwe kwa lugha ya kiswahili ili wanafunzi waweze kujivunia utamaduni wao.*

***Mapendekezo kwa Wanahabari***

*Kwa wakati huu ambapo Kiingereza ndio kinatumika kama lugha ya kufundishia masomo mbalimbali basi wajitahidi kujifunza lugha hii kwa juhudi na maarifa ili waweze kuelewa masomo yao vizuri.*

***Kazi Tangulizi kuhusu Historia ya Kiswahili***

*Kiswahili ni lugha yenye historia yake thabiti tangu wakati wa ukoloni, na hata kabla yake. Pia lugha yenye historia na maendeleo baada ya kupatikana uhuru kwa mataifa ya Afrika Mashariki, ambapo ndipo kilipo kitovu cha matumizi yake.*

*Historia ya kukua, kuenea na kuendelezwa kwa Kiswahili inahusishwa na biashara, dini (Ukristo na Uislamu) na utawala wa kikoloni (Waarabu, Wajerumani na Waingereza). Jina la lugha hii ya Kiswahili linatokana na mgeni wa kwanza wa kiarabu aliyefika katika pwani ya Afrika ya Mashariki karne ya kumi na nne. Kwa mujibu ya maelezo ya Whiteley (2015:35) ni kuwa:*

***Ufafanuzi wa Dhana Muhimu***

*Wataalamu mbalimbali wamejaribu kueleza maana mbalimbali za "neno" lugha. Zifuatazo ni baadhi tu ya hoja za Wanaisimu kuhusu maana ya lugha: Robert Lado, (2015) katika kitabu chake cha Language Testing anadai kuwa: Lugha ni chombo cha kuwasilana miongoni mwa binaadamu wa jamii moja na utamaduni wao wa namna moja. Lugha kwa upande wake na undani wake inahusiana na kuwasiliana kwa kusema na kusikia. Kwasababu hii, lugha hutumia alama kwa njia za kusema na kusikia, ambazo ni nasibu katika kuambatana kwazo na maana maalumu.*

***Lugha ya Kiswahili katika vyombo vya habari***

*Kiswahili kinatambulika kama lugha ya Afrika Mashariki. Kwa miaka mingi sasa imekuwa ikipata hadhi ya lugha ya Kimataifa, licha ya kwmba imekuwa ndio njia kuu ya mawasiliano baina ya watu wa makabila tofauti. Sifa hizi zote ni ushahidi wa haraka tu kwamba Kiswahili ni lugha ambayo imeweza kujenga misingi maalum ya maarifa ya wazungumzaji wake. Hii inatokana na kuwa hizi ni sifa zinazodhihirisha kuwa Kiswahili kinaweza kuzielezea dhana tofauti za watu wa aina mbalimbali na zikaeleweka kwa wazungumzaji wengine na hivyo watu kuelewana.*

***Hitimisho***

*Kwa kuzingatia uzoefu, historia, mapitio ya vitabu na nadharia zilizopo juu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli za nchi huru za Kiafrika hususani, Uganda, Kenya na Tanzania au katika kutoa habari katika vyombo vya habari kama vile runinga, magazeti, intanenti nakadhalika, mtafiti wa tasnifu hii anahitimisha sura hii kwa nadharia tete zifuatazo: Kinadharia, hakuna sababu muafaka inayokifanya Kiswahili kisianze kutumika katika vyombo vya habari.*

***Mapendekezo***

*Kutokana na utafiti huu, mtafiti anapendekeza kuwa Kiswahili kitumike katika kutolea vyombo vya habari kutokana na kuwa wananchi wanaposikiliza kwa lugha mbalimbali tofauti wanashindwa kupata lugha moja ya kuiendeleza taifa ya uganda.*

***Tamko la Serik`ali kuhusu Matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika vyombo vya habari***

*Mtafiti alitembelea ofisi mbalimbali za vyombo vya habari na kuhojiana nao ambapo jumla ya watalaamu sitini aliowatembelea walisema Lugha ya Kiswahili inafaa kutumika kutolewa habari vyomboni vya habari, ambapo matokeo yalikuwa kama ifuatavyo, asilimia 80 walisema inafaa, asilimia 05 walisema haifai kutumia kiswahili kama lugha ya kutolewa*

*habari na asilimia 15 walisema lugha zote ni sawa. Tamko la serikali kuhusu matumizi ya lugha ya kiswahili katika shughuli za umma. Kiswahili ndio lugha pekee ambayo huzungumzwa na kueleweka na idadi kubwa zaidi ya watanzania nchini kote.*

***MAREJELEO***

*Abdullaziz, M. (2021). "Sera ya Ikolojia ya Taifa ya Lugha ya Tanzania". E.*

*Polome na C. Hill (waha.) Lugha nchini Tanzania. OUP.*

*Amuru, K. (2017). "Jukumu la Kiingereza katika Elimu katika Afrika Kusini Mpya" katika*

*Lagos juzuu ya. 13, Windhock. Barrett J. (2018) "Kwa nini Kiingereza bado ni Kiini cha Elimu katika Shule za Sekondari Tanzania? Lugha, Utamaduni na Mtaala 7/1.*

*Besha R, Tpappes-Lomax H, na Mcha Y. (2016). "Kubadilisha Lugha Media".*

*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mimeo.Besha, R. (2015).'Lugha ya Kiswahili hivi Leo, hasa katika Siasa ''KISWAHILI Bogonko S. (2017). Tafakari ya Elimu katika Afrika Mashariki. Nairobi, OUP. Criper C. na Dodd N. (2021). "Ripoti juu ya Ufundishaji wa Lugha ya Kiingereza na yake. Tumia kama Medum katika Elimu". Dar es Salaam, Mimeo. Criper, C. na Dodd, W. (2015) "Report on the Teaching of English Language and its use as a Medium of Instruction in Tanzania". Dar es Salaam, The British Council. Fishman, J. A. (2020) Isimujamii na Matatizo ya Lugha ya Nchi Zinazoendelea'. Fishman na Wenzake (wahar.) (2019) Matatizo ya Lugha ya Mataifa yanayoendelea: 3-16. Fishman, J. A. (mhar.) (2021). MASOMO Katika Sosholojia ya Lugha, Mounton Fishman, J. A., Ferguson, C.A. & Das Gupta, J. (wahar.) (2018). Matatizo ya Lugha ya Mataifa yanayoendelea. New York, Wiley. Haugen, E. (2016). Upangaji Lugha katika Norwe ya Kisasa'. Fishman (mhar.) (2019): Joseph, J. E. (2014). Ufasaha na Nguvu - Kupanda kwa Viwango na viwango vya Lugha Lugha. London, Frances Printer (Wachapishaji).*